

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO NYUMBA SACOOS

REG: 1904

SERA YA MFUKO WA TAHADHARI.

1) UTANGULIZI.

Huu ni mfuko unaowahusisha wanachama wote wa Nyumba Saccos ambao wanatimiza wajibu wao, kwa kuchangia akiba, kumiliki hisa na kukopa mikopo kutoka kwenye chama. Mfuko huu utazingatia kukinga majanga kwa mwanachama anaposhindwa kurejesha mkopo kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake.

Mfuko huu ni tofauti na matengo ya lazima ambayo yapo kwa mujibu wa sheria ya ushirika, Mwanachama atakatwa asilimia moja (1%) katika kila mkopo atakao ukopa.

2) MADHUMUNI YA MFUKO

Madhumuni makubwa ya mfuko ni kufidia hasara inayoweza kutokea kwa NYUMBA SACOOS Kwa mwanachama atakapokuwa amepatwa na ulemavu wa kudumu ambao utamfanya ashindwekupata kipato. Aidha mfuko utatumika kutoa rambirambi kwa mwanachama atakayefariki au kufiwa na mwenza wake au mwanaye wa kuzaa [Biological child]

3) UMILIKI WA MFUKO.

Mfuko utamilikiwa na NYUMBA SACOOS LIMITED.

4) UCHANGIAJI WA MFUKO HUU.

Mfuko utachangiwa na wanachama wote wanaokopa mikopo katika SACOOS kwa kila mkopo Kulipiwa kinga ya asilimia 1% ya mkopo. Kiasi hiki hakitarejeshwa kwa mkopaji atakapo maliza kurejesha mkopo wake wote.

5) HIFADHI YA FEDHA ZA MFUKO.

Fedha za mfuko zitafunguliwa akaunti maalum katika benki, na hazitatumika kwa namna nyingine tofauti na madhumuni yaliyokusudiwa.

6) MAFAO YATOKANAYONA MFUKO HUU:

- 1) NYUMBA SACOOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari, utasimamisha makato ya mkopo wa mwanachama aliyekatwa makatopo ya asilimia (1%) ya mkopo wake kama tahadhari endapo atafariki au kupata ulemavu wa kudumu uliohibitishwa na daktari kabla ya makato ya mkopo wake hayajamalizika, ulemavu wa kudumu ambao utasababishia kutokuwa na uwezo wa kupata kipato.
- 2) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACOOS LTD atafariki, NYUMBA SACOOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa, itamkabidhi mrithi wa marehemu kiasi cha Tsh.200,000/= kama rambirambi ya SACOOS kwa familia ya mwanachama (mrithi aliyehandikwa na mwanachama katika kitabu cha mwachama).
- 3) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACOOS LTD atafiwa na mwenza wake, NYUMBA SACOOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa / itampa mwanachama aliyefiwa, kiasi cha Tsh.200,000/= kama rambirambi (si lazima mwanachama awe amechangia).

- 4) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACOOS LTD atafiwa na mtoto wake wa kumzaa [Biological child] NYUMBA SACOOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa /itampa mwanachama aliyefiwa na mtoto wake ,kiasi cha Tsh.100,000/=
- 5) Rambirambi itatolewa kwa wanachama wote wa NYUMBA SACOOS waliochangia na wale ambao hawajachangia mfuko wa tahadhari wawe wameweka akiba si chini ya miezi sita.

7) UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI PAMOJA NA NYARAKA ZA KUAMBATANISHA.

- a) Mwakilishi wa mwanachama au mwanachama mwenyewe, mwenzi wa mwanachama Atatakiwa kutoa taarifa za kifo au ajali iliyotokea na kumsababishia ulemavu wa kudumu Au kufiwa na mke au mtoto ndani ya kipindi cha miezi mitatu toka kifo au ajali husika ilipotokea na taarifa hizozitaletwa kwenye ofisi ya chama.

- b) Nyaraka na vithibitisho vitakavyohitajika kama ushahidi ni kama vifuatavyo;

- 1) Kwa mwanachama aliyefariki au kupata ulemavu wa kudumu na alikuwa na mkopo.
 - i.Nakala ya cheti cha kifo/hati ya mazishi au uthibitisho wa Afisa mtendaji kata au kijiji au chetu cha daktari kuthibitisha ulemavu wake.
 - ii.Salary slip ya mwezi aliofariki/kupata ulemavu wa kudumu.

- 2)Kwa mwanachama aliyefiwa na mwenzi wake

- i.Nakala ya cheti cha kifo au mazishi.

- ii.Barua ya mtendaji wa serikali za mtaa inayothibitisha kwamba mhusika amefariki.(Kwa mwanachama /mwenza) aliyefia kijijini mahali ambapo hati ya kifo au cheti cha mazishi hakiwezi kupatikana.

- iii.Nakala ya cheti cha ndoa iliyopitishwa na hakimu au mwanasheria.

- 3.Kwa mwanachama aliyefiwa na mtoto wake

- i.Awe ni mtoto wake wa kumzaa (Biological/Nuclear child)

- ii.Nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyopitishwa na hakimu au mwanasheria.

- iii.Nakala ya hati ya kifo au hati ya mazishi na kama amefia kijijini barua ya Afisa Mtendaji

4.Mwanachama atakayetoa taarifa za uwongo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake,ikiwa ni pamoja na kulipa adhabu ya asilimia kumi(10%) ya baki ya mkopo wamwanachama .

8.MAJUKUMU YA BODI JUU YA MFUKO

- 1.Bodi itahakiki makusanyo ya fedha ya tahadhari ikilinganishwa na mikopo iliyotolewa kwa kipindi husika.

2.Kabla ya maamuzi ya kufikia mikopo husika ,usahihi na uhalali wa mkopo na janga vitathibitishwa kwa vielelezo au nyaraka muhimu za wanachama husika

3.Taarifa ya matumizi na mwenendo wa mfuko ,itatolewa katika Mkutano Mkuu

Mabadiliko ya sera hii yanaweza kufanyiwa mabadiliko kulingana na mahitaji ya wakati na maamuzi ya Mkutano Mkuu wa chama.

Ndugu wajumbe wa mkutano Mkuu mnaombwa kuiridhia sera hii ili ianze kutekelezwa

Naomba kuwasilisha